
Form C1

WIZARA YA MAJI

BODI YA MAJI BONDE LA WAMI/RUVU

# UTABIRI WA HALI YA WINGI WA MAJI KATIKA MTO RUVU KWA KIPINDI CHA SIKU 10 KUANZIA TAREHE 22 JUNI HADI 2 JULAI, 2026







Imeandaliwa na;

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu

P.O. Box 826, Morogoro—Tanzania

Phone: 0800114031 / 0800114032

E-mail: barua@wrbwb.go.tz

Website: www.wrbwb.go.tz


Juni, 2026

## 1. UTANGULIZI

**Yaliyomo**


1. UTANGULIZI
2. ATHARI
3. UTABIRI WA HALI YA MAJI
4. USHAURI
5. HITIMISHO


Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu imeandaa na kuwasilisha utabiri wa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kuzingatia vituo vilivopo katika *Catchment* (**Kielelezo Na.1**) kwa kipindi cha kuanzia tarehe 22 Juni hadi 02 Julai, 2026. Utabiri huu unalenga kuwezesha wadau wa Mto Ruvu katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ujenzi, Viwanda, Utalii na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira kufahamu mwenendo wa wingi wa maji katika mto huo. waweze kujua hali ya mwenendo wa wingi wa maji. Aidha, utabiri huu umezingatia utabiri wa hali ya mvua na Joto zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).




Kielelezo Na.1: Vituo vilivyotumika kufanya utabiri wa wingi wa Maji katika *Catchment* ya Mto Ruvu

### 1.1 ATHARI ZINAZOWEZA TOKEA


Wingi wa Maji kwa sasa uko chini ya wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu (2009-2024), hali inaweza kusababisha yafuatayo; -

i. Upungufu wa maji kwa sekta tajwa kutokana na kupungua kwa wingi wa maji katika Mto Ruvu.

## 2. UTABIRI WA HALI YA MAJI

Utabiri wa hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu umefanyika kwa siku kumi zijazo kuanzia tarehe 22 Juni hadi 02 Julai, 2026 kama inavyoonekana katika Jendwali Na. 1; -

**Jendwali Na. 1: Utabiri wa hali ya wingi wa maji Mto Ruvu.**

| Jina la Mto | Utabiri wa Hali ya Wingi wa Maji | Kielelezo |
|---|---|---|
| Ruvu | Utabiri unaonesha kuwa wingi wa maji unaendelea kupungua kutokana na uhaba wa Mvua katika safu za Milima ya Uluguru. Aidha, kiwango cha maji kilichopo kwa sasa na utabiri wa siku kumi zijazo inaonyesha wingi wa maji uko juu ya wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu (2009–2024).<br>Pia, kiwango cha maji kilichopo kwa sasa ambayo ni lita 52,000 kwa sekunde pamoja na matarajio ya siku kumi zijazo (Lita 43,000 kwa sekunde) ni himilivu na kinatosheleza mahitaji ya sekta mbalimbali, ikiwemo mahitaji ya maji ya majumbani yanayohudumiwa na mitambo ya DAWASA ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Kwa sasa, mahitaji ya maji ni lita 6,000 kwa sekunde. (**Kielelezo**). |  |

## 3. USHAURI KWA SEKTA MBALIMBALI

Bodi inapenda kuwashauri watumiaji wa Maji katika sekta ya Kilimo, Ujenzi, Madini, Utalii, Mifugo na uvuvi, Mamlaka na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira kuchukua tahadhari dhidi ya kupungua maji katika Mto Ruvu.

## 4. HITIMISHO

Bodi itaendelea kutoa taarifa ya mwenendo wa wingi wa maji kila baada ya siku kumi na kuwahabarisha watumiaji na Mto Ruvu ili waendelea kuchukua hatau za tahadhari dhidi ya kuongezeka/kupungua kwa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa siku zijazo.